BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Tano – Tarehe 04 Disemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Biashara na Viwanda:

Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Hoja ya kuja na Mkakati unaotekelezeka wa kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa zao la Mwani.

Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis:

Hoja ya Mjumbe kuhusu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Viti Maalum vya Wanawake kufaidika na fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

26. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (JIMBO la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    (a) Soko la Darajani kwa siku linakusanya shilingi ngapi.

    (b) Soko la Darajani lina visehemu au vipenu au vibaraza vingapi vyote kwa jumla kuanzia nje ya soko, ndani ya soko la samaki pamoja na sehemu ya kuuzia ndizi.

    (c) Je, Wizara haioni imefika wakati kutafuta M-bia ili usimamizi uwe mzuri na Serikali ipate mapato yake kikamilifu.

117. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Itakumbukwa kwamba ni mwaka umepita tangu suala la ugatuzi kuanza kutekelezwa Zanzibar kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo bado kuna malalamiko juu ya upatikanaji wa haki kwa baadhi ya watumishi wakiwemo walimu na madaktari kupitia Halmashauri husika. Aidha, uwezo wa baadhi ya maofisa wa Halmashauri kuzisimamia taaluma za wito kama uwalimu na udaktari unawatia shaka hasa kutokana na kauli zao kwa wafanyakazi hao.

    (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuziwezesha Halmashauri zetu kuweza kumudu changamoto hizo.

    (b) Je, Serikali ina mpango gani kuzipatia Halmashauri wafanyakazi wenye ujuzi wa kutosha katika kusimamia elimu na afya.

Wizara ya Fedha na Mipango:

33. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiweka mikakati mbali mbali ya kiuchumi ili kuongeza mapato ya nchi. Hata hivyo, imekuwa ni kawaida kwa vituo vyote vya mafuta kuuza mafuta bila ya kutoa risiti hali ambayo inaleta hofu kwamba kuna upotevu mkubwa wa mapato.

(a) Je, kwa nini Serikali inasita kuanzisha uuzaji wa mafuta kwa kutumia mashine za EFD.

(b) Ni kiasi gani cha mafuta kinauzwa kwa mwezi mmoja kwa Zanzibar.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

68. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imepata fungu la Bilioni Tatu kwa ajili ya vijana kwa shughuli mbali mbali za maendeleo.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha hadi sasa kimepatikana.

(b) Je, ni maeneo gani ya vijana hao yaliyofaidika

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

87. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika vipaumbele vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2018/2019 ni kuimarisha huduma za dakhalia zote za Unguja na Pemba kwa kuzipatia usafiri dakhalia mbili na kusaidia gharama za chakula kwa wanafunzi wote wanaokaa dakhalia.

(a) Je, suala hili limefikia wapi.

(b) Je, usafiri huo tayari umepatikana.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

98. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Naipongeza Serikali katika juhudi zake za kudhamini na kuhakikisha mambo ya kale hayapotei katika historia ya Zanzibar. Mambo ya kale yapo mengi sana ikiwemo ngoma, sanaa, mavazi, maeneo ya historia, utamaduni wa mzanzibari na mengi mengineyo.

(a) Je, nini madhumuni ya Serikali kuunda Idara ya Mambo ya Kale.

(b) Je, ni mambo gani ya kale yaliyopewa kipaumbele kwa Serikali ili kuhakikisha kuwa yanatambulika na kufikia lengo lililokusudiwa.

(c) Je, ni changamoto gani zinazoikabili Idara ya Mambo ya Kale ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Wizara ya Afya:

45. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali inajitahidi kuimarisha huduma ya afya ili wananchi wapate huduma hiyo bila ya usumbufu. Hata hivyo, madaktari na wafanyakazi wengine wa sekta hiyo hupangiwa kufanyakazi vijijini na badala yake kushindwa kufika kwa utaratibu mzuri, ama kutokufika kabisa katika sehemu zao za kazi na kupelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi.

(a) Je, ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya wafanyakazi wenye tabia kama hizo.

(b) Ni wafanyakazi wangapi wa sekta ya afya wamebainika na tabia kama hizo.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

94. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Kwa kuwa ujumbe wa Mei Mosi 2018 ulisema: Njia pekee ya kuanza uzalishaji na kuimarisha huduma ni kujadiliana na kujali ushirikishwaji. Na kwa kuwa taasisi yako ilipanga kuzifikia wastani wa taasisi 600 kwa mwaka 2017/2018 kupitia Kamisheni ya Kazi.

(a) Je, hadi sasa ni taasisi ngapi zimekaguliwa na kuona dhana ya ushirikishwaji wa wafanyakazi inatekelezwa.

(b) Je, hatua zipi zitachukuliwa kwa zile taasisi zitazoshindwa kutekeleza dhana hio muhimu.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

5. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

Hivi karibuni Serikali imeunda Kamati ya Mawaziri ya kufuatilia Migogoro ya ardhi, kamati ambayo inafanya kazi zake vizuri. Hata hivyo imeonekana kuwa baadhi ya viongozi Serikalini wanahusika kusababisha migogoro hiyo ya ardhi kwa kutoa vibali au kuwapa amri wahusika kutoa vibali vya ujenzi na uvamizi wa maeneo ya ardhi.

(a) Je, hatua gani zitachukuliwa na Serikali kwa baadhi ya viongozi wanaojihusisha na migogoro ya ardhi.

(b) Je, endapo watendaji watalazimishwa kutoa vibali vya ujenzi au kuuzwa kwa maeneo ya ardhi kinyume na utaratibu, hatua gani watachukuliwa.

(c) Kwanini Serikali inaruhusu wananchi wapatiwe ardhi wajenge na baadae wanawavunjia wakati tayari wameshatumia gharama kubwa za ujenzi huo.

20. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Hivi karibuni kumekuwa na upandaji wa bei ya mafuta na kusababisha pia gharama za usafirishaji na maisha kupanda kisingizio kikiwa ni kupanda gharama za usafirishaji katika bandari ya Dar es Salaam na soko la dunia.

(a) Je, Serikali haina njia mbadala ya uingizaji mafuta nchini kwa gharama nafuu ili kuwapunguzia mzigo wananchi ambao bei za mafuta zinavyopanda zinawaumiza.

(b) Je, utaratibu wa mwanzo ulikuwaje mpaka mafuta yalikuwa yanapatikana kwa bei rahisi.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

31. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliunda Kamati Maalum ya kufuatilia tatizo la usajili wa meli za Kimataifa kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA) ili kupata ukweli kama kuna uvunjaji wa sheria.

(a) Je, Zanzibar imepoteza kiasi gani cha fedha tangu kuzuiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika zoezi hilo la usajili wa meli.

(b) Je, vigezo gani vimetumika Zanzibar kuzuiwa kusajili meli za Kimataifa kupita Ofisi yake ya Dubai wakati makosa ya usafirishaji wa dawa za kulevya au silaha wanatakiwa kushtakiwa wamiliki wa meli kwa mujibu wa Sheria za Nchi ambako tukio limefanyika.

(c) Kwa kuwa hizi ni Wizara (2) tofauti ya SMZ na SMT na kila moja ina sheria zake, hatuoni umefika wakati suala hili likaangaliwa upya.

74. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Je, ni lini ujenzi wa jengo la Terminal 3 utakamilika.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

39. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Katika kipindi cha mwezi wa Septemba na Oktoba, 2018, kulikuwa na upungufu wa bidhaa ya mchele ambao ndio chakula kikuu hapa Zanzibar. Na kwa sababu hiyo mchele ulipanda bei hadi kufikia shs. 1,400/- kwa kilo bei ya jumla, jambo ambalo halikua sahihi kwa wafanyabishara wetu kuongeza bei hio kwa visingizio tofauti.

(a) Je, kitu gani kilichosababisha kuongezeka kwa bei ya mchele.

(b) Ni sababu gani iliyopelekea kuadimika bidhaa hiyo nchini kwa mara moja.

(c) Je, Wizara ilichukua hatua gani kukabiliana na wafanyabiashara ambao walipandisha bei ya mchele.

III. TAARIFA ZA SERIKALI:

Waziri wa Biashara na Viwanda:

Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Azimio la kuitaka Serikali kuja na Mkakati unaotekelezeka wa kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa zao la Mwani.

IV. HOJA YA MJUMBE:

Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis:

Hoja ya Mjumbe kuhusu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Viti Maalum vya Wanawake kufaidika na fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo.

Zanzibar,
04 Disemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.